




## Metaphorical depiction in Siti Binti Saad's songs



Research Article



Published in Nairobi, Kenya by Royallite Global in the *Research Journal in African Languages*, Volume 3, Issue 2, 2022

© 2022 The Author(s). This article is distributed under a Creative Commons Attribution (CC-BY-NC-SA) license.

### Article Information

Submitted: 16<sup>th</sup> March 2022

Accepted: 29<sup>th</sup> May 2022

Published: 20<sup>th</sup> June 2022

Additional information is available at the end of the article



<https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/>

To read the paper online, please scan this QR code



### Juma Nyongesa Job

Department of Lanhuages, Pwani University, Kenya

Email: [jayjuma52@yahoo.com](mailto:jayjuma52@yahoo.com)

<https://orcid.org/0000-0001-9105-8686>

### Abstract

This paper sought to examine the importance of context in the Siti Binti Saad's songs. How does the context assist in the creation of the theme and the stylistic devices? Several songs have been used to answer the above question. Siti Binti Saad grew up during the colonial period and in the last times of slave trade. Colonial time is one of the factors of context that can be depicted from Siti's songs. This paper has also vividly by examples outlined how metaphors are created in the reverence of context. Context plays a big role in the creation of imagery and the metaphors. It will be of help if the singer or the writer of literal work can understand the context of his audience.

**Keywords:** context, imagery, metaphor, semiotic




### How to Cite:

Job, J. N. (2022). Metaphorical depiction in Siti Binti Saad's songs. *Research Journal in African Languages*, 3(2). Retrieved from <https://royalliteglobal.com/african-languages/article/view/857>





## Mandhari na muktadha katika mafumbo aliyoyatumia Siti Binti Saad kwenye nyimbo zake



Published in Nairobi, Kenya by Royallite Global in the *Research Journal in African Languages*, Volume 3, Issue 2, 2022

© 2022 The Author(s). This article is distributed under a Creative Commons Attribution (CC-BY-NC-SA) license.

### Article Information

Submitted: 16<sup>th</sup> March 2022

Accepted: 29<sup>th</sup> May 2022

Published: 20<sup>th</sup> June 2022

Additional information is available at the end of the article



<https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/>

To read the paper online, please scan this QR code



### Juma Nyongesa Job

Chuo Kikuu cha Pwani, Kenya

Barua Pepe: [jayjuma52@yahoo.com](mailto:jayjuma52@yahoo.com)

<https://orcid.org/0000-0001-9105-8686>

### Ikisiri

Makala hii imeshughulikia dhana ya mandhari katika nyimbo za Siti Binti Saad. Ni jinsi gani mandhari yalikuza maudhui na mtindo wa mafumbo katika nyimbo za mtribu huyu. Siti aliwasilisha masuala mbalimbali katika nyimbo zake. Masuala haya yalijitokeza kwa ujenzi wa mandhari. Mifano mbalimbali ya nyimbo imetolewa kutosheleza maelezo haya. Siti alikulua katika karne ya ishirini na moja. Wakati ambapo kulikuwa ni mwisho wa utumwa na mwanzo wa ukoloni katika mataifa ya Afrika Mashariki. Hali hii ya ukoloni pia ni moja wapo ya vijenzi vya mandhari katika nyimbo za Siti. Siti aliweza kukuza taswira ya mandhari ya jambo lingine kwa kusudi ya kuzungumzia suala lingine tofauti. Kazi hii imeonyesha jinsi taswira ya mandhari tofauti inaweza kukuza mitindo mingine mafumbo yakiwemo. Makala hii imekomaza umuhimu wa wanafasihi kuweza kuzingatia mandhari ya msomaji na mwimbaji katika kazi za fasihi. Mwimbaji ili aweze kuelewa hadhira anafaa afahamu mandhari ya hadhira yake. Mandhari ndiyo hutengamanisha mwimbaji na hadhira yake.

**Maneno muhimu:** mandhari, taswira, fumbo, semiotiki

### How to Cite:

Job, J. N. (2022). Mandhari na muktadha katika mafumbo aliyoyatumia Siti Binti Saad kwenye nyimbo zake. *Research Journal in African Languages*, 3(2). Retrieved from <https://royalliteglobal.com/african-languages/article/view/857>

**Utangulizi**

Tangu miaka ya 1980 usomaji wa mafumbo umeachwa kuangaziwa kama jambo la mtindo wa kishairi hadi nyenzo ya mantiki katika isimu na katika sayansi (Steen, 2015:315). Kwa sasa mantiki huonekana kama jambo la ufasili katika jamii zetu. Mantiki ni jambo la fikira na ufasili katika jamii. Hii inamaanisha kuwa ni lazima mtu awe na uwezo wa kuelewa jamii husika ya mwandishi au mwimbaji ndipo awe na uwezo wa kufasili kazi yake ifaavyo. Nadharia ya Semiotiki inasisitiza kuwa, uelewaji wa utamaduni wa jamii ya msanii ni muhimu sana. Ndiposa Lakoff na Johnson (1980:3), wanasisitiza jambo hili kwa kusema kuwa mafumbo ni dhana ambazo tunaishi nazo katika mazingira yetu ya kila siku. Kwao watu wengi huchukulia mafumbo kama kipashio cha ushairi chenye lugha nzito wala si jambo la kawaida katika maisha. Wanapinga imani kuwa mafumbo ni kwa lugha tu. Wanaliona kama dhana ya lugha, fikira na matendo. Wanadai kuwa katika tafsili zetu za kimsingi au za kawaida kwa jinsi ambavyo tunafikiria na kutenda kawaida hujitokeza kimafumbo. Kwa hivyo, ni wazi kuwa mafumbo hutathimini jinsi ambavyo tunachukulia ulimwengu huu. Iwapo fasili yetu ni ya kimafumbo basi tunafikiria kwa yale ambayo tunapitia. Ndiposa Lakoff na Johnson, (1980:4) wana mfano wa fumbo la mjadala kuangaziwa kama vita, *'Debating is war'*.

Wanasema kuwa iwapo mjadala hautazamwi katika jamii zingine kama vita basi jamii hizo haziwezi kuelewa fumbo 'mjadala ni vita'. Wanasema kuwa iwapo jamii hizo pengine kwao mjadala ni kama densi ambayo ni ya kufurahisha na haina ushindani kwa hakika fumbo hilo litakosa maana katika muktadha wa matumizi. Kwa msingi wa msimbo wa kiutamaduni wa nadharia ya Semiotiki na maelezo ya akina Lakoff na Johnson (1980) na Steen (2015), ni muhimu mandhari, muktadha na utamaduni unaojitokeza na alimoimbia nyimbo za Siti kuweza kueleweka. Sehemu hii ililenga kuonyesha jinsi mandhari yameingiliana na mtindo wa mafumbo. Aidha, kuonyesha suala la fumbo mfumbie mjinga mwerevu atalingamua, jinsi hutokea. Sehemu hii imeangaza au kufafanua mandhari yaliyomo katika nyimbo za Siti za Taarab kwa kuzingatia namna mafumbo yalivyowasilishwa.

Mandhari ni mahali au makazi maalum yaliyojengwa na mtunzi na mnamotukia matokeo mbalimbali ya kazi ya fasihi. Njogu na Chimerah (1999), wanasema kuwa mandhari ni mazingira ya wahusika pamwe na matukio, na yanahusu mahali wanamokaa wahusika na kuingiliana, mazingira ya kijamii na kiuchumi ya wahusika hao na nafasi zao za kitabaka. Wanaendelea kudai katika kufahamu mandhari kunatusaidia kuelewa hisia, imani, tabia na maumbile ya wahusika. Mandhari huwa sura ya mahali au sehemu ambapo matukio ya hadithi au masimulizi hutokea. Mahali ambapo matukio hujitokeza huwa panachukuana na wakati.

Kea (2011), ameeleza muktadha kama mazingira. Muktadha ndio kila jambo katika fasihi, hudhibiti maana katika mawasiliano, bila muktadha huwezi kuzungumza vizuri. Ikiwa ujumbe wako utawasilishwa kwa muktadha fulani na ueleweke katika

muktadha mwingine ni jambo tofauti. Kwa kiwango fulani neno muktadha linaweza kutumika kama mbadala wa neno mandhari lakini ni vizuri idhihirike kuwa mandhari huwa ni mapana sana kwa mfano mandhari katika tamthilia ni jambo tofauti hasa katika maandalizi ya jukwaa. Kwa hivyo, si wakati wote ambapo neno muktadha litatumika sawa na mandhari. Kwa hivyo, muktadha ni sehemu ya mandhari.

Arasa na wengine (2017), wanasema kuwa kuna aina mbalimbali ya mazingira ambayo huweza kuathiri uandishi wa mtunzi. Katika utafiti wetu ni uimbaji. Wanatoa aina hii ya mazingira kama ya kisiasa, kijamii, uchumi na mahali. Ni vizuri ieleweke kuwa mafumbo ya Siti Binti Saad yalijitokeza katika muktadha wa ngoma za jamii ya Waswahili za Taarab. Twomey (2016), naye anatambua aina mbili kuu za miktadha ya fasihi. Anatambua muktadha wa mwandishi na muktadha wa msomaji. Twomey (ashatajwa) anasisitiza kuwa ni muhimu mtu kufahamu muktadha wa mwandishi alipokuwa akiandika kazi yake kabla ya kuihusisha na muktadha wake. Kwa kazi yetu itakuwa bora iwapo tutaangazia muktadha wa mwimbaji Siti Binti Saad. Miktadha hii inaweza kuwa sawa au tofauti na ya wasikilizaji wa nyimbo zake. Twomey (2016), anaendelea kutaja miktadha mingine. Muktadha wa kijamii ni pale ambapo vipengele vya kijamii vinajitokeza kwa mfano suala la ndoa, matambiko na hata mavazi. Katika muktadha huu wa kijamii anatambua kuwa kuna muktadha wa kijamii wa mwandishi na muktadha wa kijamii wa msomaji au msikilizaji.

### **Mifano ya mandhari katika mafumbo aliyoyatumia Siti kwa nyimbo zake**

Wimbo *Nauliwani* unahitaji msikilizaji kuuhusisha na matokeo yaliyopelekea Siti kuimba wimbo huu ili kuuelewa. Kulitokea mtafaruku kati ya Siti na Bwana Subeit. Siti alijiona kama mwanamke dhaifu na hakupenda jinsi ambavyo alikuwa amechukiwa na Subeit. Subeit alikuwa mmoja wa waimbaji wake na alikuwa amemchukulia Siti kama mwanamke mbaya. Katika wimbo huu Siti anajirejelea kama kidege. Ili msikilizaji afahamu fumbo ‘kidege nauliwani’ ni lazima aelewe muktadha wa kutoelewana kati ya Subeit na Siti. Mfano katika wimbo *Nauliwani Kidege* (uk. 258):

*Nauliwani kidege nauliwani*  
*Sili cha mtu sinani kidege nimefanyani*  
*Nauliwani kidege nauliwani*

Msikilizaji ni lazima arejeele kisa hiki ndipo afahamu mafumbo yanayojitokeza. Siti anatambulisha mandhari yake kwa kusema kuwa ‘jelebi motomoto natafuta pesa mbovu’. Katika fumbo hili Siti aliashiria kuwa yeye alikuja mjini kufanya biashara ya kutafuta pesa na biashara yake ni uimbaji. Mfano katika ubeti:

*Jelebi motomoto natafuta pesa mbovu*  
*Jamani Mombasa ipo maua yanaliwa*  
*Na ndege ondoka ukalinde maua yanaliwa na ndege*

Katika ubeti huu Siti anatambulisha kuwa wanawake wabaya wapo Mombasa. Usemi huu unajitokeza kwa fumbo ‘jamani Mombasa ipo maua yanaliwa’. Kuliwa kwa maua ni jambo baya.

Maua katika jamii za Kiafrika hutumika kama kitambulisho cha mandhari mazuri. Vilevile, maua katika miti huzaa matunda. Maua yakishachanua matunda huwa yapo karibu kujitokeza. Ndege anapokula maua anaharibu kuchipuka kwa matunda. Ndege ndiye watu wabaya ambao Siti anarejelea.

Wimbo *Hili Shairi Ihwani Nataraji* unadhihirisha umuhimu wa kuelewa mandhari ya mwimbaji. Wimbo huu unaanza kwa fumbo la nyoka. Nyoka anayerejelewa hapa ni mpenzi mbaye amebadilika akawa hatari kama nyoka mnyama. Mwimbaji katika wimbo huu anahofia mpenzi wake anaweza kumuathiri. Anasema kuwa, “Huyu nyoka ni sumu katika nyama”. Fumbo hili linatambulisha hatari ya sumu kwa kitu kitamu. Bibi huyu amekuwa kero kwa mapenzi ambayo yalikuwa yakinawiri vizuri. Matumizi ya nyama na nyoka ni viashiria vya mandhari ambavyo lazima vifahamike vizuri kwa hadhira. Msimbo wa urejelezi wa nadharia ya Semiotiki unasisitiza umuhimu wa kurejelea maana ya vitaja katika jamii husika ndipo vitajwa vieleweke. Kwa mfano katika wimbo huu *Hili Shairi Ikhan Nataraji*, iwapo hadhira itakosa kuwa inatoka kwenye jamii ya kushabikia kitoweo cha nyama haitafahamu hali ya sumu kuwa kwenye kitoweo hiki. Mfano katika wimbo huu *Hili shairi Ikhan Nataraji* (uk. 245):

*Ihwani nataraji kutamka  
Mebaini mambo yaliyonifika  
Fahamu kila anofuga nyoka  
Huyu nyoka kumbe huwa mazoweya  
Kumwuweka ni adha ilotimiya  
Mesumbuka ya Rabii tusahiliya  
**Huyu nyoka hafai kutendwa wema**  
Hutoweka ambawo mwalazima  
**Hugeuka akataka kukuuma**  
Huyu nyoka hafai kutwendwa wema  
Himshika kwa imani na huruma  
Na kuondoka sijui yake hatima  
Huyu nyoka nalimkunjuwa  
Afrika na thamani nikatowa  
Kwa hakika lakini sikumjuwa*

Ishara ya ‘nyoka kugeuka na kutaka kumuuma mwenyeji wake’. Ni fumbo ambalo linadhihirika wazi kwa watu ambao wana ufahamu wa mnyama nyoka. Hatari ya nyoka kutaka kumuuma mtu, ni ya kuogofya. Ishara hii inahusishwa na mwanamke ambaye anataka kumdhuru mpenziwe. Bwana huyu anasema kuwa mwanamke huyu hafai kutendewa mema. Mwanamke huyu hastahili kupendwa amegeuka katili.

Nadharia ya Mtindo inatambua ukiukaji wa matumizi ya msamiati. Waimbaji hutumia msamiati kutoka sajili mbalimbali ili kuunda mafumbo kwa miktadha tofauti na sajili iliyotumika. Msamiati hujitokeza kama mafumbo kwa kuwa huwa umetumika kwa sajili tofauti au miktadha tofauti na ule wa kawaida kwa matumizi. Kwa mfano,

Wimbo *Kitabu Achore*, unazungumzia tendo la ndoa siku ya fungate lakini msamiati ni wa muktadha wa elimu. Utamaduni wa Kiislamu mwanamke ni lazima adhihirike kama ni bikira kabla ya kufungishwa ndoa. Hali hii ilipelekea tendo la ndoa kufanywa siku ya harusi. Taswira ya kuchora inatumika kuasilisha dhana ya tendo la ndoa. Msamiati uliotumika hapa ni wa elimu, kitabu na kalamu hutumika katika masuala ya elimu. Mfano katika wimbo *Achore Kitabu* (uk. 255):

*Eeee leo achore*  
*Eeee leo achore*  
*Bwana harusi asema*  
*Ataka kitabu achore*  
*Na kalamu ashachonga*  
*Ataka kitabu achore*

Mafumbo katika nyimbo za Siti yanaweza tu kueleweka vizuri kwa misingi ya utamaduni wa Kizanzibari ya hapo awali wala si ya kisasa. Siti aliimba nyimbo hizi wakati wa ukoloni katika jamii za Afrika. Wakati huu hakukuwa na haki kwa Waafrika; haki ilikuwa kwa Waarabu na Wazungu katika enzi hizo. Dhuluma kwa Waafrika lilikuwa jambo la kawaida kutendwa na Wazungu hawangeshtuka hata chembe. Nasra katika mahojiano naye alikiri kuwa wakati huo, nyimbo za Siti zilivuma kwa sababu ziliangazia masaibu ambayo yaliwatatiza Waafrika wa tabaka la chini.

Fasihi kwa ujumla hukuzwa kwa vipengele vyake vikuu; fani na maudhui. Nadharia ya mtindo inasisitiza mwingiliano uliopo kati ya mtindo na maudhui. Kando na vipengele hivyo kukuza fasihi, sehemu hii ililenga kudhirisha kuwa vipengele vya fasihi hukuzana na huendelezwa na mandhari. Katika wimbo wa Siti *Kitendawili Tega* (uk. 242), maudhui ya udanganyifu na ulafi wa wanaume yanajengwa. Siti anajenga mwanamume mlaifi mwenye sifa za fisi. Mfano katika ubeti:

Kitendawili tega, usambe naona uoga  
Ushindani nayo, misoga shamba linatia mbega  
Kitendawili tega, usambe naona uoga

Fisi ni mnyama ambaye ana tabia za ajabu. Fisi hatulii sehemu moja, yeye haridhiki na chakula anachopata, kila mara anatamaa ya kupata zaidi. Fisi mara nyingi huvamia chakula cha mwenyeji na kuhuhamia kwingine na kuvizia. Siti anamtambulisha fisi huyu kama laghai. Sifa hizi anazihusisha na mwanamume mlaghai kwa wanawake. Wanawake wametambuliwa kama mizoga ambayo fisi analenga. Fisi ana tamaa kwa mizoga hii. Kwa hivyo, wakati wa harusi wanawake hutahadharishwa kuhusu wanaume wenye tamaa kwa wanawake.

Masuala haya ya mafumbo na mandhari yanahusu namna wenyeji wanavyotangamana na wanavyoshughulikia maisha yao kwa ujumla. Hali kadhalika kwa kuwarejelea Maitaria na Wafula (2018:74), wanaokubaliana na msimbo wa

kiutamaduni wa nadharia ya Semiotiki kuwa uwasilishaji wavipengele vya fasihi hutegemea tajiriba ya mtunzi kama mmoja katika jamii hiyo. Kwa hivyo, mtunzi kwa njia nyingine ni kiwakilishi cha jamii nzima. Kwa maana hii, nyimbo za Siti zinaweza kuwa kielelezo cha maisha ya wanajamii wa Uswahilini katika enzi zake na hata sasa. Nyimbo zake hizi ni kama viashiri vya utamaduni asilia katika jamii ya Waswahili.

Vilevile, ushairi wa Kiswahili kama ulivyo katika tanzu muhimu za fasihi, hauibuki katika ombwe tupu. Ushairi huu ni zao halisi la jamii na ni nyenzo za kuhifadhi na kuwasilisha utamaduni wa wenyeji. Nadharia ya Semiotiki inasisitiza kuwa katika lugha kuna vitu viwili ambavyo ni : kitaja na kitajwa. Kitajwa ni alama inayochukua na kirejeele, yaani maana iwakilishwayo na alama hiyo. Mahusiano ya viwili hivi ni ya kubuni tu, hutegemea utamaduni wa jamii husika. Kauli hii inaungwa mkono na msimbo wa nadharia ya Semiotiki wa kiutamaduni kuwa kupitia kwa tungo za msanii, hadhira hupata viashiria vinavyohusu itikadi na maono ya mtunzi kwa kuzingatia muktadha wa utamaduni wa jamii husika. Kwa hivyo, mtunzi wa fasihi hususani ushairi wa Kiswahili, huwa na msukumo au kichocheo kinachomwongoza katika uwasilishaji wa tungo zake. Kichocheo hicho, ndiyo sababu ya kuchukulia kuwa tungo za fasihi ni kioo cha jamii. Zaidi ya hilo, tamathali hizo ni viashiria elekezi na viashiria ugwe muhimu vinavyoteuliwa na wenyeji kwa kuzingatia tajiriba yao ya maisha na utamaduni wao. Kwa ufupi ufundi wa Siti Binti Saad kwa njia nyingine ulitokana na utamaduni wa jamii yake. Mjadala huu unatuelekeza kuwa matumizi ya mafumbo kwa wingi ni zao la jamii, upekee wa msanii hujitokeza kwa jinsi anavyowasilisha maana ya mafumbo katika kazi yake.

Mafumbo katika nyimbo za Siti yalituwezesha kutambua mandhari yake na kuweza kufahamu utamaduni wa Waswahili. Jambo hili lilitokea katika harakati za uchanganuzi wa mafumbo. Kwa mujibu wa msimbo wa kiutamduni wa nadharia ya Semiotiki katika ufumbuzi wa mafumbo, ni lazima: kiashiria = kiashiriwa ambayo kwetu ni fumbo = ishara. Kwa maelezo haya ni wazi kuwa viashiria ni lazima vifahamike katika miktadha ya mwimbaji na msikilizaji. Kwa mfano katika baadhi ya nyimbo za Taarab za Siti Binti Saad, lugha ya mafumbo ambayo inatumika huhusisha dhana za bahari, mito, samaki, misitu, wanyama, ndege na milima huwa ni mambo ambayo yanapatikana katika upwa wa Afrika Mashariki. Jambo hili hufanya yeyote ambaye ana ukuruba na mandhari haya kuwa na nafasi nzuri ya kuelewa dhana hizi katika Taarab kushinda yule ambaye hajatangamana na dhana za ufuoni.


Aidha, hakuna kitu kilicho na nguvu ya maana katika usemaji na utungaji kama picha. Vilevile, picha husaidia sana kuvutia hisia na huleta mguso wa hali ya juu kwa upande wa mwenye kufikiwa na ujumbe. Kwa mfano wimbo wa Taarab ambao umetungwa na kuimbiwa katika mandhari ya Pwani unaweza kuwa na maana tofauti kati ya wasikilizaji wawili, mmoja akiwa katika mandhari ya mtunzi na mwingine akiwa katika mandhari tofauti na mtunzi. Mfano katika wimbo *Jua toka* (uk. 230):

*Koroma haliwi nazi, japo litakatika  
Usipopenda mkweti, ataakasirika  
Mtawe au dalali huwezi kazi ya duka  
Jua toka jua toka  
Nianike kibandile changu, kimendondoka*

Katika ubeti huu Siti Binti Saad anatumia mandhari ya kipwani anapotumia dhana ya nazi na koroma. Ni vigumu kwa wakaazi wa bara kuelewa ushairi huu wa koroma kwa kuwa mandhari yao hayana mmea wa nazi. Jambo hili lilimpelekea King'ei, (1993) kudai kuwa ni vigumu kwa wakazi wa bara kufahamu nyimbo hizi za Taarab. Wimbo *Kijiti* (uk. 241) unao unadhahirisha hali hii. Kwa mfano:

*Tazameni tazameni, tazameni tazameni  
Alivyofanya Kijiti, alivyofanya Kijiti  
Kumchukua mgeni, kumchezsha foliti  
Kendanaye maguguni kumrejsha maiti*

Maguguni ni neno linalofahamika zaidi katika jamii ya Unguja zaidi kuliko jamii zingine katika Upwa wa Afrika Mashariki. Hii inaonyesha wazi kuwa fasihi huchota malighafi yake katika jamii husika. Hata katika wimbo huu ili uweze kuelewa undani wake ni lazima ufahamu mandhari ya mashambani na mjini. Kwa mujibu wa Mbaabu (1985), Waswahili kama jamii hupenda kuishi vijijini au mashambani, kinyume na mawazo ya baadhi ya watu ambao wamekuwa na mielekeo kwamba, jamii hii ina utamaduni wa kupenda maisha ya 'ubazazi', anasa na starehe za mjini. Kutokana na uwepo wa mimea, wenyeji wana uzoefu wa matumizi na manufaa ya mimea kama nazi. Wana uwezo wa kutambua tofauti kati ya koroma na nazi. Katika kielelezo hiki inakuwa rahisi kufahamu mandhari ya Pwani nakufumbua mafumbo.



Katika kielelezo hiki, dhana ya mandhari inadhihirika wazi kuwa ni muhimu. Kile kinachozungumziwa ni mapenzi lakini msanii ameyarejelea kama koroma. Inabidi hadhira ifahamu maana ya koroma? Ili fumbo liweze kueleweka ni lazima kitaja na kitajwa vilingane na vifahamike na



mwimbaji na msikilizaji. Kisanduku cha mkono wa kushoto kinawakilisha picha au kiwakilishi cha jambo husika ilhali kisanduku cha mkono wa kulia kinasimamia jambo lenyewe. Fumbo litakuwa fumbo ikiwa kuna ulinganuzi wa vitu viwili katika lugha iliyotumika. Vitu viwili hivi moja na kitaja na lingine ni kitajwa. Lakoff na Johnson (2003), anasema kuwa dhana muhimu katika uelewekaji wa mafumbo ni dhana inayozungumziwa na dhana lengwa. Kielelezo hiki cha fumbo katika wimbo wa *Waridi* fumbo la zombo kwenda, linalinganishwa na wapenzi kupendana katika maisha yao. Safari yao ya mapenzi iwe moja yenye maelewano na kupendana.

Fumbo ‘koroma haliwi nazi’ linatuonyesha kuwa mwanadamu daima hujikuta katika mazingira mbalimbali na maana yake inaweza ikakosa kuwa ile ambayo inafahamika katika upwa wa Afrika Mashariki. Kwa kuyachunguza mazingira hayo, binadamu hupata fikira na dhana mbalimbali kuhusu vitu viliyomo katika mazingira yake. Wakati mwingine, huhitaji kuzieleza fikira na dhana hizo kwa wengine. Mwanadamu hufanya hivyo kwa kutumia mafumbo. Mtazamo huu wa kueleza mazingira kwa viashiria hufanya mafumbo kujitokeza kama chombo cha kuyawasilisha mawazo yale binadamu aliyonayo akilini mwake kwa wengine. Mafumbo hujengwa na maneno na maneno huwakilisha mawazo. Hivyo, mwanadamu hutumia mafumbo kuelezea mawazo aliyonayo. Lakini maneno ayatumia mwanadamu kichwani hayana budi kuchukuliwa na hadhari. Kwa kuchukua jinsi yalivyo, zinaweza zikapatikana fikira kwamba uhusiano uliopo baina ya neno na dhana ni ule wa neno moja kuwakilisha dhana moja au kwamba uwiano uliopo baina ya maneno na dhana ni ule wa 1:1. Fikira za namna hii zina matatizo yake kwani inawezekana kabisa neno moja likawakilisha dhana zaidi ya moja au maneno mengi yakawakilisha dhana moja. Kwa mfano nyimbo *Nauliwani* na *Wewe Paka* zina mafumbo ambayo yanawakilisha dhana moja. Katika wimbo *Nauliwani* kuna fumbo ‘kidege’ lenye maana ya mtu wa tabaka la chini sawia kimaana na fumbo ‘paka’ katika wimbo *Wewe Paka*.

Aidha, mara nyingi imetokea kwamba mtu anaweza kukiona kitu akilini mwake lakini akashindwa kupata maneno ya kukielezea iwapo hadhira yake haitamwelewa au akose kitajwa mahususi. Wimbo *Kigalawa* ni mfano mzuri wa wimbo ambao maana ya neno moja linaweza kupata maana tofauti. *Kigalawa* ni chombo cha majini lakini kundi la Siti Binti Saad liliamini kuwa wimbo huu ulikuwa na maana tofauti na ni vigumu maana moja kujitokeza.

Wimbo *Muhogo wa Jang’ombe* una matumizi ya mafumbo ya muhogo na nazi ambayo yanatokana na shughuli za ukulima za jamii hii. Kwa mfano muhogo ni lazima upandwe na upaliliwe, si mmea wa kujiolea tu. Vivyo hivyo, nazi hupandwa katika mandhari ya Kipwani. Matumizi katika wimbo:

*Muhogo wa jang’ombe e, sijauramba mwioko*  
*Msitukane wakunga, na uzazi ungaliko*  
*Kamfunge kamfunge, beberu wa Athuman*  
*Umfunge umfunge, pahala panapo jani*  
*Endaye tezi na omo, atarejea ngamani (uk. 229)*

Fumbo lingine ambalo limejifunga katika mandhari ya Kipwani ni fumbo la methali ya mwenda tezi na omo marejeo ni ngamani katika wimbo wa Muhogo wa Jang'ombe. Methali hii inafahamika vizuri na wakazi wa Pwani. Methali hii ina matumizi ya sehemu katika vyombo vya majini. Ina sehemu ya omo, tezi na ngamani. Kutokana na uzoefu wa Siti kwa masuala ya majini kama uvuvi na vyombo vya majini na ukuruba wake na lugha ya Kiswahili kinachozungumzwa kule Unguja ana uwezo wa kutumia fumbo hili la kimethali.

Schnitzer na Pedreira (2005), wanaunga mkono madai ya Lakoff na Johnson (1980), kwa kusema kuwa matumizi ya mafumbo si jambo jipya au la kipekee ila ni jambo la kawaida katika matumizi ya lugha na ndiyo msingi wa uzoefu wa mwingiliano wa ulimwengu na binadamu. Wanasema kuwa matumizi ya mafumbo ni jambo la lazima katika maisha ya binadamu kwa sababu ya uhusiano uliopo kati ya mafumbo na mandhari. Mafumbo yakitumika sana baadaye hubadilika na kuwa lugha au misemo ya lugha ya kawaida. Wanadai kuwa mafumbo mengi hubadilika na kuwa misemo.

Mwimbaji anaweza ibua maana mpya kwa neno ambalo linawakilisha kitaja, kinachotoka kwenye mandhari yake. Kwa mfano, wimbo *Muhogo wa Jang'ombe*, muhogo ni mmea ambao unajulikana sana katika mazingira au mandhari ya Pwani. Picha ya mmea huu imo akilini mwa wasikilizaji wa eneo la Kipwani na wanaelewa taswira inayojengwa kupitia kwa mmea huu. Kwa hali hii Siti Binti Saad anaamua kujenga maudhui yake kwa fumbo la mmea huu. Fumbo hili mwimbaji anajenga kwa kuzungumzia jambo ambalo haliruhusiwi kutajwa moja kwa moja na jamii yake. Anarahisisha uelewaji wa fumbo hili la muhogo kwa kulieleza kwa fumbo lingine la 'sijauramba mwiko'. Taswira iliyopo hapa ni ya maandalizi ya kitoweo cha muhogo. Muhogo unaweza andaliwa kwa njia mbalimbali lakini njia maarufu katika sehemu ya Pwani ni ya kuupika kwa kutumia tui ya nazi. Maandalizi haya ya muhogo kwa tui ni tamaduni ya jamii ya Waswahili na huwa ni chakula maarufu sana katika jamii hii. Chakula hiki kando na kuwa kitamu huwa na sifa ya kushibisha mtu kwa haraka na huongeza nguvu za kuweza kufanya kazi za sulubu. Muhogo uliopikwa unaweza kuula bila mshirikisho wa chakula kingine au ukishirikishe kwa kukila kwa nyama au hata samaki. Kwa hivyo, wazo kuu katika maelezo haya ni kuwa utamu wa kitoweo cha muhogo unahusishwa na utamu wa pombe kutoka eneo la Jang'ombe.

Mafumbo ya kuhusishwa au ya kulinganishwa huwa ni bora mtu afahamu muktadha wa jamii husika. Kwa mfano utapata mafumbo ya kijamii yanayohusisha jinsia ya kike na yale yanayohusisha jinsia ya kiume. Jamii ya Waswahili hutambulisha mwanamke kwa fumbo husishi kama ua la waridi. Siti katika wimbo *Waridi* anamrejelea mwanamke kama waridi. Maana ya mafumbo haya yanaendana na maana ya sifa za mimea au wanyama ambazo zimehusishwa na jamii hii. Kuna sifa ambazo hufanya mnyama fulani au mmea fulani kuhusishwa na wanawake au wanaume. Iwapo sifa za mmea huo zinaendana na sifa za mwanamke, mmea huo huhusishwa na mwanamke na vivo hivo ikiwa sifa zake zinahusishwa na mwanamume. Ikumbukwe kuwa sifa hizi hufungamana na jamii husika japo zingine ni za ujumla. Waswahili wana namna ya kueleza

mwono ulimwengu wao. Sharif (1988), anasema ikiwa kabila ni watu wenye lugha maalum na fasihi iliyotokana na mawazo ya watu hao, tamaa zao na utu wao basi lugha hiyo yaani Kiswahili, ina mambo hayo na ni chombo kinachowatumikia watu wenye ngano zao, nyimbo zao, mashairi yao na mitindo mingine ya tungo mbalimbali zikiwa na mapokezi au za maandishi.


Maitaria na Wafula (2018), wanachangia kwa mjadala kwa suala la mandhari na maana ya mafumbo kwa kusema kuwa mafumbo ni utanzu unaobeba dhana ya utata ambayo huweza kuwa kikwazo kwa hadhira kufafanua na kuelewa kilichokusudiwa katika mafumbo hayo. Jambo hili hufanya jamii isifaidike na ujumbe uliomo kwenye utanzu huu wa nyimbo za Taarab. Hata hivyo, utata huu unaweza kuchanganuliwa na kuwekwa wazi kupitia taswira zinazochomozwa na mafumbo husika na hadhira kunufaika. Wanasema kuwa fumbo gumu hufumbuliwa kwa kuangalia vidokezo au vielekezi vinavyoiwezesha hadhira kupata taswira sahihi itakayoleta jibu sahihi la fumbo husika. Kitajwa hubeba kitu chenye sifa zinazokifanya kushabikiana na kitu kingine kinachopatikana katika mazingira halisi na wakati ambao upo. Kwa maelezo haya, ni wazi kuwa Siti kama mwimbaji alihusisha mandhari katika kazi yake. Vielekezi katika muktadha huu ni kama samaki ambao wanafungamana na upwa wa Afrika Mashariki. Mafumbo katika ubeti wa wimbo *Jua Toka* (uk. 230) yanaashiria haya:

*Koroma haliwi nazi, hata likatikatika  
Sigombane na mkwezi, japo akikasirika  
Mzoweya udalali, hawezi kazi ya duka*

Ubeti huu una mafumbo kama koroma, mkwezi na udalali ambayo ni mambo yanayopatikana katika mandhari ya Pwani. Fumbo la mkwezi hasa linafungamana na shughuli za uvuvi ufuoni. Kwa mujibu wa nadharia ya Semiotiki, mafumbo ya kijamii na tamaduni yanaeleweka iwapo: maana ya dhana tajwa inaeleweka na jamii, maana ya dhana taja au husishwa inaeleweka na jamii. Aidha, maana ya dhana tajwa na taja inalinganishwa kwa sababu dhana hizi zinahusiana na kufanana. Siti Binti Saad katika wimbo *Bomwanzani wa mahaba* (uk. 234) anaibua fumbo 'yeye atakuwa nyama na bwana yake kisu'. Mfano katika ubeti:

*Mimi nitakuwa nyama  
Wewe kisu wewe kisu  
Aaah aaah mimi nyama*

Uhusiano wa nyama na kisu unajulikana vizuri. Kisu mara nyingi hukatakata nyama kabla ya kuandaliwa. Kisu huwa ni kikali sana na kina madhara kwa nyama. Tukirejelea msingi wa nadharia ya mtindo, fumbo la 'kuwa kisu' lina dhana taja ya usumbufu wa bwana na dhana tajwa ya makali ya kisu. Kwa hivyo dhana hizi zinaweza husishwa na kulinganishwa na maana kupatikana. Kielelezo kifuatacho kitatufaa kuelewa jinsi jamii hutangamana na mafumbo.



Kielelezo hiki kinatambulisha picha akilini mwa msemaji ikilingana na picha akilini mwa hadhira, ishara itakuwa moja na maana ya fumbo ikiwa inafanana. Lakini picha akilini mwa msemaji na akilini mwa hadhira zikitofautiana maana inakuwa tofauti. Hali hii inasisitizwa na nadharia ya Semiotiki kuhusu maelewano katika tamaduni ya hadhira na msanii. Itakuwa bora ikieleweka kuwa fumbo linaweza kuwa moja lakini maana kwa hadhira ziwe nyingi kwa sababu ya tofauti ya picha walizonazo kuhusu fumbo hilo.

Nyimbo zingine za Siti bado zinafungamana na matendo ya kisasa. Kwa hivyo, mafumbo yaliyomo katika nyimbo za Siti yanapata picha inayoeleweka. Nyimbo ambazo zinafungamana na masuala ya ndoa kama wimbo *Ya Laiti* bado maarufu sana kwa wafuasi wa Siti. Kuna mafumbo ambayo yanafahamika sana katika muktadha wa nyimbo za taarab na katika upwa wa Pwani. Mojawapo ya mafumbo hayo katika nyimbo za Siti ni fumbo la 'kumbe wewe Paka shume', katika wimbo *Pakistani*. Matumizi ya fumbo hili yanafahamika sana kwa sababu ya uhusiano uliopo kati ya mwanamume asiyetulia katika ndoa na paka shume. Pakashume ni paka ambaye hujifanya mzuri lakini ana tabia ya kuzururazurura akiiba vyakula vya wenyewe. Fumbo hili hufanya watu wengi kufurahia wimbo huu kwa jinsi ambavyo wanaelewa na kufumbua fumbo husika. Pia kwa sababu ya fumbo kushabikiana vyema kwa vielekezi vyake. Kitaja na kitajwa vinahusiana vizuri na hufanyamaana kujitokeza vizuri. Pakashume ana tabia tofauti na paka wa kawaida. Paka wa kawaida ana sifa za upole na kutulia kwa mwenyeji wake. Paka huyu huwa hana pupa ya kuondoka nyumbani, kila mara hupatikana nyumbani.

Mfano huu wa uelewaji wa mafumbo kwa urahisi unaashiria kuwa maana ya fumbo hupatikana katika akili ya mwimbaji na msikilizaji. Maana hii hutokea baada ya mtagusano kati ya mtu

na ulimwengu wake ambao ni mandhari yake na matukio mbalimbali katika miktadha mbalimbali. Mtagusano wa binadamu na tabia ya paka shume ni rahisi kwa hadhira ya wimbo huu wa Siti Binti Saad, *Ya Pakistani* kueleweka. Siti anahusisha tabia za paka shume na mwanamume ambaye hajatulia katika ndoa na kueza kuelewa kupata maana ya fumbo hili. Kwa mujibu wa lugha wakati mwingine huwa ni ya picha pamoja na ishara. Fumbo likitokea mtu hupata taswira fulani ya picha akilini mwake. Picha ya akilini ndiyo hujenga maana ya mafumbo katika fasiri ya wasikilizaji. Kwa mfano wimbo *Koti na Suruali* ulioimbwa kukaribisha utamaduni mpya katika jamii ya Zanzibari. Wageni walikuwa wakifika Zanzibari kwa mavazi yaliyokuwa tofauti na ya jamii ya Zanzibari. Jamii hii ilitambulika kwa mavazi ya buibui na kanzu. Buibui na Kanzu katika akili ya wakaazi wa Unguja iliakilisha watu wenye imani na mila za Kiislamu. Lakini koti na suruali ziliwakilisha imani ya watu wageni wenye imani na tamaduni tofauti na za Unguja wakati huo. Mzee Ameir Bin Ameir Bin Sudi katika mahojiano naye alisema kuwa ilikuwa ni lazima mwanamke kuvaa buibui katika umma huko unguja. Lakini wageni walifika kwa suruali na koti, utamaduni tofauti wa mavazi ya uswahilini. Mfano katika ubeti wa wimbo *Koti na Suruali* (uk. 243):

*Koti na Suruali si haramu  
Hasa avae Bwana ende zamu  
Wapende umtazame wishe hamu  
Koti...`*

Katika ubeti huu Siti anajenga mafumbo yake kwa kutumia mandhari mpya. Ni wazi kuwa Siti anafahamu vizuri koti na suruali ni nini. Kwa hivyo, kupitia kwa ufahamu huu anahusisha ujumbe wa utamaduni mpya Zanzibari. Hili ni jambo muhimu pia kwa yule ambaye anahitaji kupata ujumbe huu. Ni lazima awe anajua utamaduni wa awali wa mavazi kule Unguja na utamaduni wa mavazi ya wageni. Ndiposa Lakoff na Johnson (1980), wanasema kuwa mafumbo huwa katika akili ya mtu. Mandhari pia huathiri imani ya mtu, Siti kama mhusika kwa misingi ya nafsi ya kwanza katika wimbo *Ya laiti* ni wazi kuwa mandhari ya Siti Binti Saad katika jamii ya Uislamu yalimwaathiri. Kwanza katika wimbo wake anaanza na ishara ya kuamini kuwa ndoa inahitaji kudumu milele pengine kwa talaka. Mfano katika ubeti wa wimbo *Ya laiti* (uk. 232):

*Yalaiti napenda pasi kifanii  
Tofauti sikutilii moyonii  
Sikuachi leo na kesho peponi*

Kupitia fumbo hili la ‘sikuachi leo na kesho hadi peponi’, Siti anaashiria imani yake ya kumpenda mumewe hadi mbinguni. Imani hii inaelezwa kupitia kwa mafumbo ‘sikuachi leo na kesho peponi’. Wimbo mwingine ambao una imani ya mwenyezi Mungu kama inavyofungamana na dini ya Kiislamu ni wimbo *Jua Toka* (uk. 230):

*Mungu akitaka kupa, hakuletei barua*  
Mungu akitaka kupa, hakuletei barua  
*Hukupa usingizini pasi wewe kujua*  
*Kwenda mbio si kupata, bure unajisumbua*

Wimbo huu unataja imani kuwa baraka ambazo watu hupata maishani hutokana na mwenyezi Mungu si kwa pupa ya binadamu. Fumbo 'Mungu akitaka kukupa hakuletei barua' ni athari ya imani ya dini ya Kiislamu kwa mwimbaji. Mwimbaji ana imani kuwa baraka za Mwenyezi Mungu hazitangazwi zikija. Huja kwa ghafla bila mtu kutarajia kamwe.

Athari hii ya mandhari ya kidini ya Kiislamu inajitokeza katika wimbo wa Beru. Katika wimbo huu, mwandishi anataja baadhi ya mavazi ambayo yanaashiria imani yake au ya mandhari yake. Kwa mfano katika fumbo la 'muhimu ila kaniki, buibui kukataa'. Fumbo hili linaashiria kuwa Siti amelelewa katika mandhari ya Uislamu. Buibui ni vazi ambalo huvaliwa na wanawake kama njia ya kustiri miili yaokwa umma. Kaniki ni vazi la kufanyia kazi. Mavazi haya ni kitambulisho cha utamaduni wa Waislam katika upwa wa Afrika Mashariki. Nyonje (2016:19), anasema kuwa mavazi hutueleza filofia na ujumi wa jamii husika. Kwa hivyo muono wa imani ya dini ya Kiislamu unajitokeza katika fumbo hili.

Imani ya utu, heshima na mapenzi ya dhati ni moja wapo ya athari za kidini ambazo Siti alizipata katika mandhari yake. Nyonje, (2016) anasema kuwa Uislam ulikataza mambo yafuatayo ambayo kila mtu mwadilifu hakutarajiwa kujihusisha nayo: ulafi, uchoyo, kiburi, wivu, ubinafsi, tamaa, ukosefu wa uaminifu na madharau kwa wengine. Falsafa hii ilisisitiza umuhimu wa mja kujitahidi aushini kufikia maadili haya yote lakini wachache waliyatimiza.

Kazi ya mwanamke katika utamaduni wa Waswahili ni ya kumtunza mumewe na watoto na shughuli zao zote hulenga hilo. Watoto walio na umri wa kati ya miaka mitatu na sita hupelekwa kwenda kusoma duksi (kufunzwa kuikariri Korani tukufu). Baadaye wanapofikisha umri wa miaka sita, hupelekwa shule za kawaida. Pia huendelea na mafunzo ya dini ya Kiislamu, madrasa. Katika madrasa watoto hufunzwa kusoma, kuandika, kuhesabu, Kiarabu na historia ya dini ya Kiislamu. Jioni wanaume wengi hukaa nje ya nyumba zao na kunywa kahawa chungu, ambayo huuzwa katika mitaa yao (Kea, 2011). Kea (ashatajwa) anaendelea kudai kuwa wanawake pia wana wajibu wa kuwafunza watoto wao hasa wale wa kike, jinsi ya kukua kama wanawake wenye heshima katika jamii yao.

Hassan (2017:60), anaainisha mbinu ya kimazingira au Toponimu kama mbinu ya kuunda majina kulingana na mazingira ya sehemu. Hali hii inaonyesha kuwa uundaji wa majina ya mitaa katika jamii ya Waswahili hutegemea vitu wanavyoviona katika mazingira yao na majina hayo huwa ni rahisi kukubalika na wazungumzaji wa lugha hiyo. Kwa mfano, Hassan (2017), anataja sehemu kama mtoni kuwepo kwa mto katika

mazingira, Kilimani kuwepo kwa kilima na kijangwani sehemu ambayo ni jangwa. Mbinu hii ndiyo wasanii wanatumia kuunda maneno na majina katika kazi zao za fasihi. Baadhi ya majina haya yanatumika na wasanii hawa katika utunzi wao wa Taarab.

Wimbo wa Siti *Muhogo wa Jang'ombe* unarejelea sehemu inayojulikana kama Jang'ombe. Jang'ombe ni neno linalotokana na mazingira. Kwa mujibu wa Hassan (2017:57), mtaa huu ni mtaa maarufu sana katika Kisiwa cha Unguja. Mtaa huo ni miongoni mwa mitaa ya mwanzo iliyokuwa ikijulikana kama ng'ambu (si mjini wala si shamba). Mtaa huu upo baina ya Magresheni ya zamani, Ziwapi polisi, Mpendae na Migombani. Asili ya jina hilo alikuwepo mzee aliyeishi Makunduchi; siku moja aliwatembelea jamaa zake wanaoishi Kilimani, wakati huo usafiri ulikuwa wa tabu sana kutoka Makunduchi hadi mjini, hivyo alipata usafiri wa msaada hadi fuoni usiku ulipokuwa umeshaingia. Alitembea kwa miguu hadi Wayani na kufika Shule ya Jang'ombe saa nne usiku.

Mja huyu alitafuta huku na kupata mti uliokuwa umelimiwa vizuri akalala. Kwa ufupi alilala kwa mawazo na uwoga. Asubuhi ilipofika alishukuru kwa kuamka salama na alikwenda kwa jamaa zake na kuwa simulia mkasa uliompata. Aliulizwa na mwenyeji wake, "Hee mwenzetu msituni ulilalaje?" Akasema nililala ja ng'ombe. Neno 'Ja' kwa lahaja ya kimakunduchi ni sawa na kama akimaanisha amelala kama ng'ombe. Habari ya mzee huyu ilienea na tokea siku ile mtaa huo ukaitwa Jang'ombe.

Mashairi ya kijiografia ni msingi muhimu wa kanuni ya ushabiki kweli katika kazi za kifasihi hususan zinazoandikwa katika mkondo wa uhalisia. Kanuni ya ushabiki kweli inasisitiza uhusiano wa karibu kati ya ulimwengu wa kiubunifu na ulimwengu halisi kwa kumfanya msomaji aweze kuamini kuwa matukio, mazingira na maingiliano ya wahusika yanayotokea katika ulimwengu huo yanaweza kukubalika. Ubeti wa tano katika wimbo *Kijiti* (uk. 241) unatambulisha haya:

*Mambo haya ni ajabu kila tukiyatizama  
Kijiti kauwa mtu na tumboni mna mwana  
Kijiti kavuka mto mashahidi wamezama*

Ubeti huu una mandhari ya mto. Mshororo wa mwisho katika ubeti huu unaashiria hali ya kuvuka mto. Picha inayojijenga ni ya kuvuka mto. Ujumbe wa kuwaua unajitokeza kupitia mandhari ya mto. Masuala ya bahari na uvuvi ni mojawapo ya mandhari ya kijiografia ambayo yalikuwa katika maisha ya Siti. Misitu na wanyama au ndege ni miongoni mwa masuala ya mandhari ya kijiografia ambayo hujitokeza katika uimbaji wa Taarab. Kuna baadhi ya Taarab ambazo mwanamke hupewa jina la nyuni, maua na wengine hata wanyama. Hali hii inatambulisha mandhari ya kijiografia ya mwandishi. Kwa kufanya hivi mbinu mbalimbali za lugha na za uandishi zinajijenga kwa misingi ya mandhari kama haya.

Kazi ya fasihi haiwezi kuwa tu historia kwa kuwa kunahitajika kutoa picha halisi ya maisha ya wakati husika, kwani japo mada ni matukio halisi ya kihistoria, namna ya

kusawiri mada hizo na matini huchukua mkondo wa kifasihi. Iwapo tutakubali kwamba kazi ya fasihi simulizi si amali ya mtu binafsi, basi tutakuwa tayari tumeonyesha kwamba fasihi na jamii ni vitu visivyotengana. Hata pakitokea kwamba maisha ya mtu binafsi yametumiwa kama nguzo ya kutunga kazi ya fasihi, hatuwezi kusahau kwamba tajiriba zake zimepaliliwa na maisha yake kama mwanajamii, awe anachukua au kukiuka maadili na matarajio ya jamii hiyo. Wimbo wa *Kigalawa* mpaka leo bado unatumika katika jamii ya Unguja kwa kuuhusisha na mfumo wa ubepari ambao huwatenganisha masikini na matajiri.

Suala la uongozi katika Zanzibari nyakati za Siti ni muhimu sana katika kuelewa mafumbo katika nyimbo zake. Siti aliishi katika mwisho wa karne ya kumi na tisa na mwanzo wa karne mpya ya ishirini, kwa hivyo alipata kupitia historia ya uongozi tofauti. Binti Saad alizaliwa wakati wa ukoloni na uongozi wa Oman kule Zanzibari. Historia hii ni muhimu hasa kwa kuelewa wimbo *Kijiti* ambapo mahakimu walitoa uamuzi bila kutegemea ushahidi. Nyakati hizo suala la haki kwa Mwafrika halikuthaminiwa sana. Wimbo *Beru* unazungumzia suala la wakati ambalo pia ni mojawapo ya vipengele vya mandhari ambapo mwanamume anahiitajika kuwajibikia familia, linajitokeza. Siti analalama kuwa mwanamume asiye na kazi ni mapepe. Ujumbe wake unajijenga katika uwajibikaji wa mwanamume kwa familia. Mandhari haya ni ya Kiafrika ambapo mwanamume ndiye mwenye kukimu mahitaji ya familia.

Mafumbo yanabaini historia ya Zanzibari kisiasa. Mfano mzuri ni wimbo *Sifa kwa Waingereza*. Wimbo huu wa bendi ulipendwa sana na uongozi wa Uingereza. Katika wimbo huu Siti anabaini kuwa ni vyema Waingereza kuchukua usukani kuwashinda Wajerumani. Siti na bendi yake wanatumia mafumbo kuonyesha mabadiliko haya kwa mfano anasema kuwa 'hajuwi pa kuketi chaka limeingia simba'. Simba anayezungumziwa hapa ni Muingereza ambaye alimshinda Mjerumani. Anaendelea kudhihirisha mabadiliko haya, kwa kusema kuwa 'milima ameilaza'. Kulaza milima ni usawa ambao Waingereza wameuleta katika Zanzibari kwa watu wa Zanzibari hasa kwa kukomesha utumwa. Mfano katika ubeti wa wimbo *Sifa kwa Waingereza* (uk. 224):

*Namsifu Mngereza na Generali Smati*  
*Bara amaitengeza meondowa tofauti*  
***Milima ameilaza kwa suudi na bahati***  
*Hawajuwi pa kuketi chaka limeingia simba*

Anaendelea kuonyesha mabadiliko ya kisiasa katika Zanzibari wakati huo anaposema kuwa ni vigumu kumuona simba kukaa na nyati. Nyati anaashiria Wajerumani ilhali simba anaashiria Waingereza. Waingereza waliwapiku Wajerumani ili kuweza kutawala himaya ya Zanzibari. Mfano katika beti:

*Aduwi wameduwaa njia kuu hawapiti*  
*Mwituni wamesawaa watakayo hawapati*  
***Ni ajabu kumwona Simba kukaa na nyati***



*Hawajui pia kuketi chaka limeingia simba*

Historia ya Uingereza kunyakuwa himaya hii ilidhihirika zaidi kwa Waingereza kuweka bendera katika sehemu za himaya hii. Ishara hii inajitokeza kwa fumbo 'Tanga na Dar es Salaam twalikuta mlingoti'. Wamitila (2003), anaeleza kwamba watunzi wa kazi za fasihi ni watu ambao huyachukua matukio na visa vinavyotokea katika jamii zao na kuviwakilisha kiubunifu katika hadithi, tamthilia, hadithi fupi na ushairi. Ubunifu huu unaashiria kuwa waimbaji na wasanii wengi huwasilisha dhamira ambazo zinatokana na mandhari yao.

**Kihitimisho**

Makala hii imewasilisha uchambuzi wa data za utafiti kulingana na malengo ya utafiti wetu. Mandhari yanavyotumika katika kujenga mafumbo ni suala ambalo limeangaziwa. Makala hii imeshughulikia umuhimu wa Siti kutumia mafumbo katika uimbaji wake wa nyimbo za Taarab. Mandhari na mitindo mingine ya kifasihi inajitokeza katika mafumbo ambayo Siti alitumia. Ni wazi kuwa mandhari ni jambo muhimu katika uwasilishaji wa kazi yeyote ya fasihi. Mandhari ndiyo hukuza mtindo, ujumbe na dhamira ya mwandishi au mwimbaji katika kazi za kifasihi. Mtindo ndiyo uti wa mgongo wa kazi ya fasihi.

**Marejeleo**

- Abdalla, A. R. (2018) *Kuchunguza Dhamira na Fani katika Nyimbo za Taarab Asilia: Mifano ya Nyimbo za Shakila Saidi Khamisi*. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Huria cha Tanzania. (Haijachapishwa)
- Acquaviva, G. (2004) *Jazanda Ya Njozi Katika Baadhi ya Mashairi ya Euphrase Kezilahabi*. Swahili Forum 11 (2004: 69-73).
- Adungo, C. (2009) *Gwiji wa taarab; Khadija Kopa*. Taifa Leo.
- Alhabib, E. A. (2012) *Matumizi ya lugha katika nyimbo za taarab*. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu Cha Tanzania.
- Ali, A. H. T. (2014) *Taashira na Utendaji katika Nyimbo za Harusi za Waswahili, Kisiwani Unguja*. Tasnifu ya Uzamifu (Ph. D) Chuo Kikuu Cha Egerton. (Haijachapishwa)
- Allen, G. (2000) *Intertextuality*: New York. Routledge 29 West 35th Street.
- Arnold, M. (1849) *The strayed Reveller and other Poems*. B Fellowers. Ludgate street.
- Askew, K. M. (2002) *Performing the Nation: Swahili Music and Cultural Politics in Tanzania*. Chicago& London. The university Chicago Press.
- Askew, K. M. (2000). 'Following the Trucks of Beni: The Difussion of The Tanga Taarab Tradition'. *Katika Mashindano: Competitive, Music Perfomance in East Africa*. Dar-es-Salaam: Mkuki na Nyota Publishers
- Babusa, H.O. (2005) *Vigezo badalia kuhusu uainishaji wa mashairi ya Kiswahili*. Tasnifu ya .A. Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (haijachapishwa)
- Bakhtin M. (1981) *Theory of the text*. London: Routledge.
- Balisidya, M. (1987). "Tanzu na Fani za Fasihi Simulizi" katika Temu, C na E. Mulika na 19, Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Bathes, R. (1994) *The semiotic Challenge*. Barkely. University of California Press.
- Beja, S. K. (2001) *Giriana Funeral Songs: A Functional Aesthetic study* Ph.D Thesis, University of Nairobi.
- Broughton, S. na wenzake. (2000). 'World Music', Makala za Taarab Zanzibar: Nyaraka za Taifa Zanzibar.
- Buffon, G. (1930) *Buffon's Discourse on style*. Paris Librarie: Hatier Publications.
- Chai, F. (2003) *Gaining access in Fieldwork*. Makala iliyoasilishwa katika warsha ya AICAD idara ya lugha na Isimu, Chuo Kikuu cha Egerton tarehe 15/11/2003.
- Chiraghdin S. na Mnyampala M. (1977) *Historia ya Kiswahili*. Oxford University Press. Nairobi.
- Coombes, H. (1953) *Literature and Criticism*. London. Chatto and Windus.
- Culler, J. *The Pursuit of signs*. London: Rotledge and Kegan Paul.
- Enon, J. (1998) *Education Research Statistics and Measurement*. Makerere University, Uganda
- Fair, L. (2013) *Historia ya Zanzibar na Nyimbo za Siti Binti Saad*. Twaweza Publishers. Nairobi.
- Fair, L. (1998) *Music, Memory And Meaning: The Kiswahili Recordings of Siti Binti Saad*.

- Swahili Forum 55: 1-16.
- Fromkin, V., Rodman, R. and Hymes M. (2003). *An Introduction to Language*. Thomson/Heinie. Boston.
- Githonga, W. N. (2013). *Uchambuzi Linganishi wa Fani na Maudhui ya Nyimbo za Harusi za Kimeru na za Kiswahili*. Tasnifu ya M.A. (Haijachapishwa).
- Hartman, C, (1980) *Free Verse: An essay on prosody*. Princeton University Press.
- Hassan, A. H. (2017). *Kuchunguza Fasihi ya Majina ya Mitaa Mjini Unguja*. Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu Cha Huria Cha Tanzania.
- Hilal, N. M. (2007). *Mfinyazi Aingia Kasri: Siti Binti Saad, Malkia wa taarab*. Mkuki na Nyota Publishers. Dar es Saalam.
- Holman, H. (1960). *A handbook to Literature*. New York. Odyssey.
- Igobwa, S. E. (2007). *Taarab and Chakacha in East Africa: Transformatio, Appreciation and Adaptation of two Popular Music Genres of the Kenyan Coast. Conference on Music in the world of Islam* 8:8-13.
- Issa, M. (1991). *Jukwaa la Taarab Zanzibar*. Helniski. Mediafrica.
- I- Wensu, L. (2002). *What can Metaphor Tell us About culture?* National Tainwan University Language and Linguistics. 3: 3: 589-612.
- Jilala, H. (2008). 'The Artist Uses of Metaphors in Constructing Meanings and Messages in New Generation Songs in Tanzania', University of Dar-es-Salaam (MA Dissertation Unpublished).
- Kahigi, K.K na Mulokozi, M.M. (1982). *Kunga za ushairi na Diwani ya Yetu*. Daressalam. Tanzania Publishing House.
- Kaneko, M. (2012). *Metaphor and Symbol*. University of the Witwatersrand
- Kimani, R. (1989). *Nguzo za ushairi wa Kiswahili*. Nairobi. Macmillan Kenya
- King'ei, K. (1993). *Language, culture and communication: The role of Swahili Taarab Songs in Kenya 1963-1990*. (Unpublished). (Ph.D) Howard
- Kipacha, A. (2015). *Taswira za Ndege katika Maandiko ya Shaaban Robert*. Swahili Forum 22 (2015:1-19)
- Khamis, W. A. (2016). *Kuchunguza Dhamira za Nyimbo za Siti Binti Saad*. Tasnifu ya Chuo Kikuu cha Tanzania. (Haijachapishwa)
- Khamis, S. A. M (2004). *Versality of Taarab in Relation to Local and Global Influences*. Swahili Forum 11. P. 3-37.
- Khatib, M. (1992). *Taarab Zanzibar*. Dar- es-salaam. Tanzania Publishing house.
- Kothari, R. (1990). *Research Methodoly: Methods and Techniques 2 edition*, New Delhi. New Age International Ltd.
- Knappart, J. (1967). *Swahili Taarab Songs*, Africa and Ubersee 50 (3): 163-172.
- Kyalo, M. J. (2012). *Mandhari katika Hadithi Fupi: Ulinganishi Diwani za Pendo la Hebana Hadithi Nyingine na Mizungu ya Manabi na Hadithi Nyingine*. (haijachapishwa)
- Lakoff, G. and Jonson M. (1980). *Metaphors we Live By*. University of Chicago Press. Chicago.

- Lanham, R. (1983). *Analyzing Prose*. New York.
- Leech, G. (2008). *Language in Literature*. London. Pearson Education Limited.
- Mturo, G. (2011) *Dhimaya Semi Zilizoandikwa katika Daladala: Uchambuzi wa Vipengele vya Lugha na Dhamira*. Tasnifu ya Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam. (haijachapishwa).
- Mohamed, S. A. (1995) *Kunga za nathari ya Kiswahili: Riwaya, Tamthilia na Hadithi Fupi*. Nairobi. Jomo Kenyatta.
- Msokile, M. (1993) *Misingi ya uhakiki wa Fasihi*. Nairobi. East Africa Education Publishers
- Mukopi, M. (2005) *Hadithi fupi ya kisasa za Kiswahili kama utanzu mahuluti*.Tasnifu ya Chuo Kikuu Cha Kenyatta (haijachapishwa).
- Munyao, K. J. na Mwangi, K. P. (2011) *Mtindo na Maudhui katika Nyimbo za Msanii John De'Mathew Nchini Kenya*. Mulika 35:114-134
- Muusya, K. (2012) *Mandari katika hadithi fupi*.Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu Cha kenyatta (haijachapishwa).
- Ndungo, C. M (2006) *The Image of Women in Afrika Oral Literature*. A case Study of Gikuyu oral Literature. Gender issues Research Report Series, No. 23.
- Ndwiga, P. N. (2013) *Mitindo Katika Mashairi ya Diwani ya Karne Mpya*. Tasnifu ya M.A . Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Njogu, K. na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*.Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.
- Nguti, M. (2013). *Ulinganishaji wa Matumizi ya Tafida za Mukadha wa Nyumbani katika Lugha ya Kikamba na Kiswahili*. Tasnifu ya M. A (Haijachapishwa).
- Nyonje, J. W. (2016) *Mwonoulimwengu Wa Waswahili: Jinsi inavyojitokeza katika ngano*. Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu Cha Nairobi.
- Ojode, O. J. (2017) *Uchanganuzi Kipragmatiki wa Sitiari katika nyimbo za Taarb: mfanano wa Mzee Yusuf na Mwanahawa Ally*. Tasnifu M. A Chuo Kikuu cha Kisii (haijachapishwa)
- Ortony, A. (1980) *Understanding Metaphors*. University of Illinois. Massachusetts.
- Oyoyo, J. O. (2010) *Uhakiki wa fani katika ngano tano za kiswahili*.Tasnifu ya M.vA Chuo Kikuu Cha Nairobi. (haijachapishwa).
- Roberts, S. (1967) *Diwani ya 3: wasifu wa Sinti Binti Saad*. Dar es Salaam. Printpak Tanzania Limited.
- Robersts, S. (1991) *Wasifu wa Sinti Binti Saad*. Mkuki wa Nyuki. Dar es Salaam.
- Ruo, K. K (1989) *Nguzo za ushairi*. Macmillan. Nairobi.
- Saleh, S. S. (1980) Taarab Unguja ( Taarab in Tanzania). *Lugha Yetu* 37: 35-47
- Sanga, I. (2016) *The Archiving of Siti Binti Saad and the her Engagement with Music Industry in Sharban Robert's Wasifu wa Siti Binti Saad*. 2: 33-44
- Sengo, T. S. Y. (2009) *Sengo na Fasihi za Kinchini*. AERA Kiswahili Research Products. Dar es Salaam.
- Simpson, P. (2004) *Stylistic: A Resource book for Students*. London.Routledge.
- Simuyu F. W. (2011) *Kitovu cha Fasihi Simulizi: kwa shule, vyuo na ndaiki*. Serengeti

- Bookshop. Mwanza.
- Shaban, M. et al. (1966) *Waimbaji wa Juzi*. Chuo Cha Uchunguzi wa Lugha ya Kiswahili. Da es Salaam.
- Sheikh, S. (1994) Yanayoudhi kuyaona mafumbo na vijembe vya Kiswahili AAP (7-11) Swahili-Kolloquium.
- Steen, G. (2015) *Metaphor and Style through Genre, with Illustrations from Carol Ann Duffy's Rapture*. Bloomsbury and Diana logo. New York.
- Takada, M. et al. A study of Metaphorical Mapping involving Socio-cultural Values: How is Woman Conceptualized in Japanese.
- Timammy, R. (2002) *Mombasa Swahili Women's Wedding Songs: A stylistic Analysis*. University of Nairobi. (Haijachapishwa).
- Traore, F. (2004) *Continuity and change in Zanzibar Taarab Performance and poetry*. Swahili Forum 11:75-81
- Trop, J. (1993) *Women and Africanization of Taarab in Zanzibar*. (Ph.D). Dissertation. School of Oriental and African Studies.
- TUKI (2004) *Kamusi ya Kiswahili sanifu*. Nairobi. Oxford University Press.
- Vierke, C. (2012) *Mafumbo: Considering the Functions of Metaphorical Speech in Swahili Contexts*. Annual Conference on African Linguistics. 42: 278-290.
- Wafula, R. (2007) *Nadharia za uhakiki wa fasihi*. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundations.
- Wambua, M. (2001) *Mtindo wa nyimbo za Kakai Kilonzo*. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Kenyatta. (haijachapishwa)
- Wamitila, K. W. (2002) *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele vyake*. Phoenix. Nairobi.
- \_\_\_\_\_ (2003). *Kamusi ya Fasihi: Stilahi na nadharia*. Nairobi. Nairobi Focus.
- \_\_\_\_\_ (2003) *Kichocheo cha Fasihi na Andishi*. Nairobi. Focus.
- \_\_\_\_\_ (2008) *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi. Vide-Muwa.
- Wanyama, A. (2006) *Maudhui na mtindo katika Kamuse utendi wa wabukusu Khusala*. Tasnifu ya Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (haijachapishwa).
- Wardhaugh, R. (2002) *An Introduction to Sociolinguistics*. (4<sup>th</sup> Ed). Oxford: Blackwell Publishers.
- Wekesa, A. (2008) *Matumizi ya taswira katika ushairi-huru wa Kiswahili*. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).
- Yego, E. (2013) *Nafasi ya Mwanamke: Jinsi inavyotetewa katika nyimbo za Taarab Zanzibar*. Tasnifu ya M. A (haijachapishwa)